



# KARATASI YA VIDOEZO KWA FAMILIA

Kusoma katika familia ni muhimu kwa kila umri. Watoto na vijana wanaweza kuunganika na familia zao wanaposoma pamoja. Mwanzoni mwa elimu ya chekechea, kusoma pamoja ni muhimu zaidi.

Watoto hupata kumaizi ulimwengu wao zaidi. Aidha, wanajifunza jinsi herufi na maneno hufanya kazi. Familia zinaweza kusaidia watoto wao wakati wanajifunza kusoma. Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ambayo unaweza kutumia wakati unaposoma vitabu katika maktaba yako ya Louisville Growing Readers

- Soma mara nyingi. Mjitolize pamoja ili kufanya usomaji kuwa na tajriba chanya. Mtoto wako anaweza kuketi kwenye paja lako au kando yako ili aweze kuona picha zilizopo. Watoto watafurahia kutumia muda wao pamoja nawe.
- Maktaba yako ya Growing Readers ina vitabu vidogo kwa sababu maalum. Vimeandaliwa kwa ajili ya mikono midogo! Mhimize mtoto wako kushika kitabu na kufungua kurasa wakati mnasoma pamoja.
- Vitabu vingi katika maktaba yako vina maneno machache katika kila ukurasa. Yatumie kumsaidia mtoto wako kuelewa jinsi vitabu hufanya kazi. Onyesha maneno wakati unayasoma. Ongea kuhusu mwelekeo wa maneno: kutoka kushoto kwenda kulia na kutoka juu kwenda chini. Bainisha nafasi baina ya maneno.
- Mazungumzo kuhusu vitabu huimarisha stadi za lugha za mtoto. Tenga muda wa kuongea na mtoto wako kuhusu kile mnachokisoma. Panga matumizi ya maneno mapya. Ongea kwa kutumia sentensi kamili. Mhimize mtoto wako kuongea, kuongea, na kuongea.
- Mpe mtoto wako nafasi ya kuuliza maswali kuhusu kitabu husika. Unaweza pia kuuliza maswali ili kumhimiza mtoto wako kutumia maneno zaidi. Tumia maswali wazi ambayo mtoto hawezi kujibu kwa neno moja tu au maneno mawili. Jaribu:
  - Nieleze kuhusu...
  - Una maoni gani kuhusu...?
  - Nieleze zaidi.
- Watoto wengi watapata vitabu wavipendavyo katika maktaba yao ya Growing Readers. Watataka kuvisoma tena na tena. Vyema kabisal! Kusoma kitabu kile kile mara nyingi kunaweza kuimarisha stadi za mtoto za kusoma na kuandika .
- Jaribu kutenga muda kila siku ambao wewe na mtoto wako mnaweza kutumia kwa pamoja mkisoma. Hii huwasaidia kutambua kuwa kusoma ni muhimu. Mtoto wako atangojea kwa hamu utararibu huu maalum kila siku.
- Usiwe na wasiwasi kuhusu kusikika mjinga au kujirudia wakati unaposoma na mtoto wako. Kwao, ni muda mzuri na wa kufurahisha kuwa pamoja!

